

## **Changamoto za Kipragmatiki kwa Wanafunzi wa Kiswahili Nchini Rwanda**

*Mukamana Helene*<sup>1</sup>

na

*Ntawiyanga Sylvain*<sup>2</sup>  
Chuo Kikuu cha Rwanda

DOI: <https://doi.org/10.56279/mulika.na42t1.7>

### **Ikisiri**

Makala haya yanalenga kuchunguza changamoto za kipragmatiki kwa wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda. Ingawa wanafunzi Wanyarwanda wanajifunza lugha hii kuanzia mwaka wa kwanza wa shule za sekondari, imedhihirika kuwa wanapambana na changamoto mbalimbali katika matumizi yao ya Kiswahili (Ntawiyanga, 2015). O'Keeffe (2011) anafafanua kuwa ustadi wa kipragmatiki ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili wanaojifunza lugha na kuwa ni vigumu kuukuza uwezo huu kwa sababu maendeleo yake hayatokani na umilisi wa kisarufi. Makala haya yameweka bayana changamoto za kipragmatiki kwa wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda, sababu au vyanzo vya changamoto hizo, na yametoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana nazo. Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Urekebishaji Mawasiliano ya Giles (1973) ambayo inaweka pamoja vipengele vya kisaikolojia na vya kijamii katika kuamua mtindo wa mawasiliano yenye mwingiliano au mtagusano wa kijamii. Mbinu zilizotumika kukusanya data za utafiti huu ni hojaji pamoja na mahojiano. Wanafunzi wa Kiswahili katika Ndaki ya Elimu, Chuo Kikuu cha Rwanda pamoja na wahadhiri wao ndio walioshirikishwa katika utafiti huu. Kulingana na uchunguzi wa data iliyotumika katika makala haya, imedhihirika kuwa wanafunzi wa Kinyarwanda hukabiliwa na changamoto ambazo hutokana na uhamisho wa mitindo ya lugha kutoka Kinyarwanda hadi Kiswahili. Aidha, imedhihirika kuwa vyanzo vingi vya changamoto hizi ni kujifunzia Kiswahili nje ya utamaduni wake, kutojali mtindo sahihi unaopaswa kutumiwa pamoja na ukosaji wa kielelezo cha kufuatilia.

### **1.0 Utangulizi**

Kiswahili ni miongoni mwa lugha zinazofundishwa nchini Rwanda na ufundishaji wake huanzia shule za sekondari hadi vyuo vikuu. Kabla ya kujifunza Kiswahili, wanafunzi huupata umilisi wa lugha yao ya asili, Kinyarwanda. Aidha, katika shule nyingi za binafsi, wanafunzi hawa hujifunza Kiingereza na Kifaransa, kuanzia ngazi

---

<sup>1</sup>Baruapepe: [mukamahela@gmail.com](mailto:mukamahela@gmail.com)

<sup>2</sup>Baruapepe: [sntawiyanga@gmail.com](mailto:sntawiyanga@gmail.com)

ya chekechea ilhali katika shule za umma ujifunzaji wa lugha hizi huanzia mwaka wa kwanza wa shule za msingi. Hivyo, wanafunzi hukutana na Kiswahili wakiwa tayari na welewa wa aina fulani katika mawasiliano yao kwa kutumia lugha ya Kinyarwanda na lugha hizo nyingine za kigeni. Cohen (2014) anadokeza kuwa mtazamo wa jamii kuhusu ujifunzaji wa lugha ni kipengele muhimu katika utumiaji wa lugha na kuwa ukuzaji wa ustadi wa pragmatiki wa lugha ya pili siyo kazi rahisi kwa wajifunzaji. Kwa kuwa baadhi ya vipengele vya utamaduni wa Wanyarwanda hutofautiana na vile vya utamadauni wa Waswahili, utafiti huu ulilenga kuchunguza ikiwa wanafunzi tajwa huathiriwa na utamaduni wa lugha yao ya kwanza katika matumizi yao ya Kiswahili.

Kati ya lugha zinazofundishwa katika mfumo wa elimu nchini Rwanda, Kinyarwanda ndiyo lugha rasmi na lugha ya taifa na hutumiwa nchini kote. Kwa hivyo, utafiti huu umejikita katika kuchunguza athari za matumizi ya Kinyarwanda katika Kiswahili kutokana na hadhi yake na kuwa ndiyo lugha yenye mnasaba mmoja na Kiswahili. Kwa mujibu wa Ntawiyanga (2015), kuna vipengele vya Kiswahili vinavyohusiana sana na vya Kinyarwanda na ambavyo ni changamoto kwa Wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunza Kiswahili. Miongoni mwa vipengele hivyo ni vile vya kiothografia, kimofolojia, kisintaksia, kimsamiati na kisemantiki. Baadhi ya maneno ya Kinyarwanda yenye mfanano wa kimuundo au kiothografia na maneno ya Kiswahili huweza kudokeza maana tofauti katika lugha hizi. Hivyo, matumizi ya maneno hayo kwa mwanafunzi humtaka awe makini katika matumizi yake ya Kiswahili. Canale (1983) anaeleza kuwa mtumiaji wa lugha hutakiwa kujenga uhusiano wa karibu kati ya miundo ya kiisimu na ile ya kimatumizi. Yeye anabainisha kuwa ujuzi wa kanuni za kisarufi hauna umuhimu wowote ikiwa mtumiaji wa lugha hana maarifa ya kimatumizi kulingana na kanuni za kijamii.

Erton (2007) anaunga mkono maoni ya Canale (keshatajwa) anapoeleza kuwa ujuzi wa lugha huambatana na uwezo wa kuitumia lugha hiyo kulingana na mazingira yaliyopo. Uwezo huu unazingatia vipengele vya kiutamaduni na kijamii ambavyo ndivyo kigezo cha kutambua ikiwa mtumiaji wa lugha ameshapata umahiri wa kimawasiliano au la. Erton anabainisha kuwa uwezo wa kimawasiliano hauzingatii tu matumizi ya kanuni za kisarufi, bali ni mchakato wa kuweka pamoja vipengele vingi vya kijamii na vya kiisimu ambavyo humsaidia mtumiaji wa lugha kufikia malengo yake. Mtumiaji mahiri wa lugha ni yule anayeweza kutoa ujumbe sahihi kwa hadhira halisi huku akizingatia wakati mwafaka wa kutangaza ujumbe huo kulingana na mahali alipo. Hivyo basi, changamoto za kipragmatiki zilizochunguzwa katika makala haya ni njia nzuri ya kupimia ikiwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu, huzingatia kanuni za kijamii za matumizi ya lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao. Wanafunzi hawa wanatakiwa kuwa na uwezo kamili wa matumizi ya lugha kipragmatiki ili kujiandaa ipasavyo kuwa walimu mahiri wa Kiswahili ambao

watafaa kuwa kielelezo kizuri cha kutumia lugha hiyo kwa wanafunzi wao baada ya kuhitimu masomo ya chuo.

### **1.1 Dhana ya Pragmatiki**

Pragmatiki ni taaluma muhimu katika ujifunzaji na ufundishaji wa lugha yoyote iwayo. Taaluma hii inafasiriwa na Massamba (2004) kama taaluma ya isimu inayojishughulisha na uchunguzi na uchambuzi wa lugha katika mawasiliano. Kwa mujibu wake, lengo kuu la pragmatiki ni kuchunguza namna lugha inavyotumiwa na wasemaji wake katika mazingira halisi, kama kwa nini msemaji anaamua kusema hivi badala ya kusema vinginevyo na anakabiliwa na masharti gani ya maamuzi. Kwa upande mwingine, Crystal (1987) anafafanua pragmatiki kama taaluma ya lugha inayojihusisha na maoni ya watumiaji pamoja na vizuizi wanavyokutana navyo wakati wa matumizi ya lugha. Pragmatiki huangalia wale wanaozungumza lugha na kile kinachozungumzwa na inajikita zaidi katika kuangalia na kuchunguza kusudi la kile kinachowasilishwa (Mnata, 2014).

Kulingana na maoni ya Crystal (1987), Massamba (2004), na Mnata (2014), pragmatiki ni kipengele muhimu cha isimu ambacho huchunguza lugha katika miktadha ya watumiaji wake. Kwa maneno mengine, taaluma ya pragmatiki huchukuliwa kama lugha katika matumizi ambapo lugha inachunguzwa kupitia matumizi yake katika jamii husika. Kulingana na umuhimu wa pragmatiki katika umilisi na matumizi ya lugha yoyote iwayo, ni lazima ishughulikiwe vilivyo katika uwanja wa ujifunzaji na ufundishaji wa lugha hiyo. Hivyo, uchunguzi wa changamoto za kipragmatiki kwa wanafunzi Wanyarwanda ni jambo muhimu katika uendelezaji na uimarishaji wa matumizi ya Kiswahili nchini Rwanda. Wanafunzi hawa hujifunzia Kiswahili katika mazingira ambayo hawapi fursa za kukitumia nje ya darasa kwani shughuli nyingine nyingi huendeshwa kwa lugha ya Kinyarwanda au Kiingereza ambacho ndicho lugha ya kufunzia masomo mengine.

Ustadi wa kipragmatiki huzingatia ujuzi wa isimu pragmatiki na pragmatiki jamii. Isimu pragmatiki hujihusisha na vifaa halisi vya kutenda dhima ya lugha na inahusu umilisi wa wazawa wa lugha katika matumizi yake mbalimbali. Kwa upande mwingine, pragmatiki jamii inajihusisha na matumizi ya lugha katika miktadha mbalimbali ambapo vifaa vya kiisimu pragmatiki hutekeleza majukumu (Taguchi, 2011). Hivyo, pragmatiki jamii hujishughulisha na matumizi ya lugha kulingana na utamaduni wa jamii. Vipengele vya isimu pragmatiki ni vile vinavyohusiana na lugha kimazungumzo kama vilivyo vipengele vya kileksika na vile vya kisintaksia. Vipengele vya kimawasiliano visivyo vya kileksika ni kama kiimbo, kidato, kimya, tabia, ishara za mwili na umbali baina ya mzungumzaji na msikilizaji.

### **1.2 Nafasi ya Pragmatiki katika Matumizi ya Lugha ya Pili**

Wananapragmatiki mbalimbali wamefanya tafiti kuhusu changamoto za kipragmatiki kwa wanafunzi wa lugha ya pili. Allami na Naeimi (2011), walionesha

mtindo wa lugha ya kukataa unaotumiwa na wanafunzi wa Kiingereza kutoka Irani. Bardovi na Mahan-Taylor (2003) wanabainisha changamoto za ufundishaji wa pragmatiki kwa wanafunzi wa lugha ya pili kwa ujumla. Barron (2003) alichunguza pragmatiki katika matumizi ya lugha kadhaa. Blum-Kulka (1997) alionesha mtindo wa kimawasiliano unaotumiwa wakati wa kupata chakula kati ya marafiki kutoka jamiilugha tofauti. Brown na Levinson (1992) walitafiti kuhusu mawasiliano ya kutumia lugha ya staha kati ya watu wanaotoka katika nchi tofauti. Castillo (2009) alitafiti kuhusu umuhimu wa pragmatiki katika ufundishaji wa lugha ya pili. Cohen (2014), alichunguza mchango wa kuongezeka kwa tathmini ya uwezo wa kipragmatiki.

Hata hivyo, tafiti hizi zilitilia mkazo kwa ujumla kuwa watumiaji wa lugha hutofautiana na kuwa mitindo ya lugha ni tofauti lakini hazikuonesha bayana athari za changamoto za kipragmatiki kulingana na mazingira ya watumiaji wa lugha zenye mnasaba mmoja kama ilivyo kwa Kiswahili na Kinyarwanda. Kwa hivyo, utafiti huu ulifanywa katika lugha ya Kiswahili na ulilenga kuchunguza changamoto za kipragmatiki za wanafunzi Wanyarwanda wanaojifunzia Kiswahili katika mazingira ya utamaduni ulio tofauti na utamaduni wa Waswahili.

Cohen (2014) anabainisha vigezo kadhaa vya kiutamaduni vya kujaribiwa kwa lengo la upimaji wa kumudu lugha kipragmatiki kwa mwanafunzi wa lugha ya pili. Hapa anajiuliza: Je, tunatarajia nini kwa mwanafunzi wa lugha ya pili ili kuhakikisha kuwa anaimudu ipasavyo lugha hiyo? Kutokana na swali hili, mtu huweza kuzingatia vipengele maalum vinavyohusiana na matumizi ya lugha pamoja na misingi ya kiutamaduni na vitendo uneni katika hali na muktadha husika. Uwezo wa kutumia dhana hizo katika mawasiliano ni ishara nzuri ya kuonesha kwamba wanafunzi wa lugha ya pili wanajenga ustadi au umilisi wao wa kipragmatiki kikamilifu.

Halikadhalika, Cohen (keshatajwa) anaorodhesha mambo muhimu ya kuzingatia katika kujenga ustadi wa kipragmatiki: uwezo wa kutoa ujumbe wa rambirambi kwa wafiwa, kushukuru, ukarimu, kuomba huduma, kuomba msamaha, kualika na mengine mengi. Hivyo, utafiti huu ulijikita katika vipengele vya kuomba huduma, kushukuru kwa huduma inayotolewa, salamu pamoja na kuaga. Uteuzi wa vipengele hivi umetokana na ukweli kwamba elimu ya kijamii ya kwanza anayopewa mtoto inahusu jinsi ya kuamkiana na kutoa shukrani (Omar, 1993). Watoto wanapokuwa wadogo hufunzwa namna ya kusalimia na kuitikia salamu. Uombaji huduma na utoaji shukrani nayo ni mambo muhimu ambayo mtoto huyazoea kuanzia wakati anapojifunza lugha yake kwa kuomba huduma ili akidhi mahitaji yake.

### **1.3 Umuhimu wa Kukuza na Kuendeleza Ustadi wa Pragmatiki**

Taguchi (2017) anafafanua kuwa kuna haja ya kuendeleza na kukuza ustadi na umilisi wa pragmatiki kwa ajili ya kuendeleza mawasiliano baina ya watumiaji wa

lughu husika. Kwake, vipengele vya kipragmatiki vinavyotakiwa kuendelezwa ni vile vya isimu pragmatiki pamoja na vya pragmatiki jamii. Vipengele hivi vinakamilishana katika kukuza ustadi wa pragmatiki wa lugha yoyote iwayo.

Taguchi (keshatajwa) anaendelea kwa kueleza kuwa umilisi wa pragmatiki unajihusisha na uwezo wa kutumia lugha na watu mbalimbali pamoja na miktadha tofauti ya mazungumzo. Kuhusu ufundishaji wa pragmatiki, Taguchi anabainisha kuwa ni vigumu kuweka mifumo rasmi ya ufundishaji katika uwanja wa pragmatiki, kwa sababu unazingatia utamadunijamii na isimujamii matumizi. Kwake, ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo katika ufundishaji wa pragmatiki: matumizi ya lugha katika muktadha wa kijamii, dhima ya lugha kimatumizi na mawasiliano kwa ujumla. Kwa mujibu wa Jung (2017), umilisi na ustadi wa pragmatiki ni mambo muhimu katika upataji wa lugha hususan lugha ya pili kwa sababu ustadi wake unachangia katika kuwasiliana na wazawa wa lugha husika.

Aidha, maoni ya Jung na yale ya Taguchi yanaonesha kuwa ujifunzaji, ufundishaji pamoja na maendeleo ya pragmatiki hutagusana na mambo kadhaa ya kutilia mkazo. Miongoni mwa mambo hayo ni utamaduni jamii, isimujamii matumizi, isimu pragmatiki pamoja na pragmatiki jamii. Kwa kumsaidia mwanafunzi wa lugha ya pili, mwalimu hupaswa kuonisha vipengele hivyo vyote ili mjifunzaji aweze kuwa na ustadi kamili wa kipragmatiki katika lugha husika. Jambo hili likitimizwa ilivyo mwanafunzi wa lugha ya pili hukuza uwezo wake wa kuongea na wazawa wa lugha ya pili husika bila changamoto yoyote.

Reigle (2011) anaweka bayana kuwa utamaduni ni kipengele cha kutilia mkazo wakati wa kuendeleza umilisi wa kipragmatiki. Kulingana na maoni yake, hatuwezi kutenganisha lugha na utamaduni na hata mtu akitaka kukuza ustadi wake wa kipragmatiki katika lugha ya pili, anapaswa kuufahamu utamaduni wa lugha husika. Hoja hii ina maana kwamba mlumbi hupaswa kuwa mwenye tamaduni mbili ama nyingi na tunaweza kusema kuwa pragmatiki inahusisha vipengele vyote vya kiutamaduni na kisosholojia katika mawasiliano ya kila siku ya wazungumzaji wa lugha husika.

Pragmatiki ni uwanja mpana unaozingatia vipengele mbalimbali vinavyoingiliana na kukamilishana katika mawasiliano. Kwa mujibu wa Reyes na wenzake (2018), uwezo wa kimawasiliano kwa wanafunzi ni mojawapo ya malengo ya ujifunzaji na ufundishaji wa lugha ya pili. Uwezo huu ndio uliozungumziwa na Allami na Naeimi (2011) wanaeleza kuwa umilisi wa kipragmatiki ni muhimu kwa mawasiliano sahihi kwa sababu kukosekana kwake huweza kusababisha kukatika kwa mawasiliano na kuwa huathiri kueleweka kwa ujumbe unaotarajiwa. Hivyo, makala haya yalitoa mwanga kuhusu changamoto za kipragmatiki ambazo ndizo huchukua nafasi kubwa katika kukwamisha mawasiliano. Umilisi wa kipragmatiki ndio huendelezwa kupitia mitazamo ya kisimujamii na ile ya kiutamaduni.

#### **1.4 Upimaji wa Ustadi wa Pragmatiki kwa Wanafunzi wa Lugha ya Pili**

Jung (2017) anaorodhesha vigezo kadhaa vya kupimia ustadi wa kipragmatiki kwa mwanafunzi wa lugha ya pili: uwezo wa kutumia vitendo uneni, uwezo wa kutumia vigezo visivyo halisi kimaana, uwezo wa kutumia dhima za staha, uwezo wa kutumia dhima za uchanganuzi usemi na uwezo wa kutumia ujuzi wa kiutamaduni katika mazungumzo.

Aidha, vigezo au vibainishi vya kiisimu na vile visivyo vya kiisimu katika mawasiliano na uwezo wa kutumia vipengele visivyo halisi kimaana ni miongoni mwa vigezo vya kupimia ubingwa wa kuzungumza lugha. Katika pragmatiki viashiria na viashiriwa hurejelewa wakati tunapochunguza maana za maneno yanayotumiwa kulingana na nia ya mzungumzaji na welewa wa msikilizaji. Hivyo, mzungumzaji au mwanafunzi wa lugha ya pili hulazimishwa kujua namna ya kuziba pengo lililopo katika maana ya sentensi na maana ya mzungumzaji na msikilizaji ili kuhakikisha kuwapo kwa uhalisi wa kilichodhamiriwa katika mazungumzo.

Vilevile, uwezo wa kutumia dhima za staha ni mojawapo ya vipengele vya kuhakikisha kuwapo kwa ustadi wa kipragmatiki katika lugha. Kwa mujibu wa Brown na Levinson (1992), kanuni za staha huwa na msingi wake katika sosholojia. Leech (1981) anaeleza kuwa staha ni kijikanuni kinachojitokeza katika misingi ya Nadharia ya Upole; inajitokeza kama njia ya kuwaheshimu na kuwasifu wazungumzaji wenza badala kujisifu ama kujitukuza mwenyewe. Ingawa kanuni hizi hupatikana katika jamii za binadamu kote ulimwenguni, matumizi yake yanatofautiana katika jamii na tamaduni kadhaa za ulimwengu mzima. Jung (2017) anatoa mfano wa tofauti hizo; anaeleza kuwa kanuni za kiutamaduni za Kigiriki huhimiza matumizi ya mtindo wa moja kwa moja katika mambo ya staha wakati kanuni za Kimarekani huchagiza kutumia mtindo usio wa moja kwa moja. Hii ina maana kwamba mwanafunzi wa Kiingereza kutoka utamaduni wa Kigiriki atakabiliana na changamoto ya kutumia kanuni zisizo za moja kwa moja wakati atakapojifunza kanuni za staha katika lugha hiyo. Mwanafunzi wa Kigiriki kutoka utamaduni wa Kimarekani kwa upande mwingine, atakuwa na changamoto tofauti ambayo ni matumizi ya kanuni za staha za moja kwa moja zinazoagizwa na jamii za Kigiriki.

Kipengele kingine muhimu katika ukuzaji na uendelezaji wa ustadi wa pragmatiki ni uwezo wa kutumia dhima za uchanganuzi usemi. Kwa kuwa ukuzaji na uendelezaji wa kipragmatiki hujihusisha na vibainishi vya kiisimu na visivyo vya kiisimu, inaonekana wazi kwamba vibainishi hivyo vinapaswa kutiliwa maanani wakati wa kujifunza pragmatiki ya lugha ya pili (Blum-Kulka, 1997). Kuoanisha vibainishi vya kiisimu na vile visivyo vya kiisimu kunasababisha mwanafunzi aendelee ustadi wake wa kipragmatiki katika mawasiliano yake. Aidha, uwezo wa kutumia uchanganuzi usemi unajidhihirisha wakati ambapo maana inayojitokeza katika lugha humtaka mzungumzaji airejelee kwa kwenda mbali zaidi ya sentensi.

Katika hali hii, uchanganuzi usemi unalenga maandishi au ishara zinazotumiwa katika mazungumzo ama matukio ya kisemiotiki. Kwa upande mwingine, ni diskosi inayohusu matini andishi au semwa kama vile maandishi ya magazeti, mazungumzo ya darasani, matangazo na ilani.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, makala haya yalinuia kudhihirisha changamoto zinazowakumba wanafunzi wanapotumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yao. Matumizi ya lugha yanaweza ama kufuata au kutofuata kanuni za kisarufi lakini watumiaji wa lugha husika wakabaki katika muktadha maalum kikamilifu, kiuamilifu na hata kiushikamano. Hivyo basi, utafiti huu ulizingatia uwezo wa kutumia dhima za staha na kutumia ujuzi wa kiutamaduni katika mawasiliano ya wanafunzi wa Kiswahili. Sehemu zilizotiliwa mkazo katika lugha ya mawasiliano ya wanafunzi ni matumizi ya salamu ambapo vitendo vya kusalimiana na kuagana vilichunguzwa, uombaji wa huduma mbalimbali na shukrani kwa huduma iliyotolewa. Uteuzi wa vipengele hivi vya kipragmatiki ulitokana na hali halisi kwamba ndivyo vinavyojitokeza zaidi katika matumizi ya lugha ya wanafunzi hawa na ndivyo msingi wa mawasiliano yao ya kila siku.

Kulingana na Ngugi (2014), kuna changamoto katika kutimiza lengo la kuamkiana kwa sababu maamkizi ni suala la utamaduni na upokezi lugha zaidi kuliko ujifunzaji. Isitoshe, utoaji shukrani nalo ni jambo la msingi linaloyatambulisha mawasiliano ya wanafunzi kwani mazingira yao huwataka waendee watu tofauti wenye nyadhifa za kuwahudumia na kutosheleza mahitaji yao. Fauka ya hayo, Kiswahili si lugha ya kwanza kwa wanafunzi Wanyarwanda. Hivyo, uchunguzi wa changamoto za kipragmatiki, athari na chanzo chake ulikuwa njia mwafaka ya kuwahimiza kutumia Kiswahili fasaha katika mawasiliano yao.

## **2.0 Kiunzi cha Nadharia**

Nadharia ya Urekebishaji Mawasiliano (kuanzia sasa NUM) iliyoasisiwa na Giles (1973) ndiyo iliyotumika katika makala haya. Kulingana na nadharia hii, vipengele vya kisaikolojia na vya kijamii huhusishwa na kuwekwa pamoja katika kuamua mtindo wa mawasiliano kwa ajili ya mwingiliano au mtagusano wa kijamii. Lengo kuu la nadharia hii ni kuelezea matatizo yanayojitokeza katika matumizi ya lugha ambapo uhamishaji lugha hupewa kipaumbele kama wasemavyo Giles na Bryne (1982). Katika maendeleo yake, nadharia hii ilitumiwa katika uchunguzi na uchanganuzi wa mambo mbalimbali kama vile tofauti kati ya matumizi na kujinasibisha na lugha ya kwanza. Hivi sasa, NUM inajihusisha na uchunguzi wa vipengele vya kiisimu na vile visivyo vya kiisimu kupimia upeo wa urekebishaji na usio wa urekebishaji katika tabia. Nadharia hii huyagusia pia masuala yanayohusiana na utambulisho wa wanajamii kwa kuzingatia mizizi ya imani, utamaduni na itikadi katika uamuzi wa matumizi ya lugha.

Kwa mujibu wa Giles (1973), mawasiliano katika lugha ya pili yanaathiriwa sana na mahitaji ya mzungumzaji ya kujinasibisha na watu wa lugha hiyo. Kujinasibisha

huko kunamsukuma mzungumzaji kuiga lafudhi na hata kubadilisha tabia yake binafsi kwa ajili ya kujifananisha na wazawa au wazungumzaji wa lugha husika. Giles anaongeza kuwa vigezo vya kiutambuzi husababisha mzungumzaji kukimbilia kubadili na kuchanganya msimbo pamoja na mabadiliko yoyote yanayoweza kujitokeza katika mazungumzo. Lengo kuu la mabadiliko hayo ni kusesitizia au kupunguza tofauti za kijamii katika mawasiliano. Mathalani, mtu akitaka kukubalika katika hali yoyote ya kijamii anapaswa kutumia mbinu makutano ambapo hujitahidi kufanikisha mawasiliano yake na watu wa jamii husika kwa kujinasibisha nao. Kwa upande mwingine, mtu akiona kuwa hana haja ya kukubaliwa na wanajamii fulani anatumia mbinu maachano ambazo humtofautisha nao kabisa.

Aidha, NUM ilisaidia kuonesha kuwa mawasiliano hayaathiriwi na kushawishiwa na vipengele vya hali ya moja kwa moja pekee, bali huathiriwa na vigezo vya kisoshoutamaduni na kijamii vya mahali ambapo mawasiliano hutokea. Hivyo, changamoto za kipragmatiki zinazowakabili wanafunzi Wanyarwanda katika mawasiliano yao ya Kiswahili zilichunguzwa. Athari za changamoto hizo nazo zilijadiliwa kwa mujibu wa desturi na utamaduni wa Waswahili. Isitoshe, Nadharia ya NUM ilichangia kubainisha kanuni zinazolingana na hali ya moja kwa moja katika mawasiliano ya wanafunzi pamoja na mambo kadhaa yanayotarajiwa na wazungumzaji kulingana na viwango vyao rekebishaji kwa lugha ya Kiswahili. Kulingana na hayo, ni vyema kueleza kuwa utendakazi wa NUM kijamii ni kama kurahisisha mawasiliano kati ya watu wa jamii tofauti ambapo mawasiliano hayo hugawika katika sehemu mbalimbali kulingana na hali pamoja na shughuli za mzungumzaji na msikilizaji.

### **3.0 Methodolojia**

Data za utafiti uliozaa makala haya zilipatikana kwa muundo changamani kwa kuhusisha mwelelekeo wa kitakwimu na wa kimaelezo. Mugenda (2008) anafafanua kuwa muundo wa kitakwimu huwa ni kama jaribio la mtafiti la kusaka na kupata data kutoka katika jamii ili kubainisha hali ya sasa ya jamii hiyo kwa kutumia kigezo kimoja au kingine. Hivyo basi, muundo wa kitakwimu humwezesha mtafiti kupata habari katika hali halisi ya wakati wa utafiti kutoka katika sampuli yake. Creswell na Clark (2011) wanaeleza kuwa muundo wa kitakwimu hulenga kumwezesha mtafiti kueleza mielekeo, maoni, tabia na sifa za jamii nzima kwa kutumia takwimu za data inayotokana na sampuli iliyoteuliwa. Katika makala haya, watafiti walikusanya data katika Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu kwa ajili ya kubainisha vikwazo vya kipragmatiki kwa wanafunzi wa Kiswahili. Fauka ya hayo, utafiti huu ulikuwa wa kimaelezo kwa kiwango kikubwa ingawa watafiti walihitaji takwimu mbalimbali kuhusu kiwango cha makosa ya kipragmatiki yaliyofanywa na wanafunzi. Baada ya kukusanya, kuchunguza na kuchanganua data, watafiti walitoa maelezo na ufafanuzi mwafaka kulingana na matokeo



waliyoyapata. Maoni ya walimu na wanafunzi yalifafanuliwa kwa kujadili mienendo na tabia za wanafunzi wa Kiswahili katika matumizi yao ya Kiswahili.

Sampuli iliyotumika katika utafiti huu ilikuwa sampuli lengwa ambapo wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili wa mwaka wa pili na wa tatu walishirikishwa kwa kupewa hojaji na/au kushiriki katika mahojiano. Uwezo wa wanafunzi hawa wa kujieleza na ule wa wahadhiri wao wa kuzitambua changamoto za kipragmatiki ambazo wanafunzi hukutana nazo ndio uliozingatiwa. Hivyo, sampuli lengwa iliyotumiwa katika makala haya ilituwezesha kupata matokeo ya utafiti huu. Best na Kahn (2010) wanaeleza kuwa sampuli lengwa humruhusu mtafiti kuteua sampuli ambayo ina wahusika wenye sifa anazozitaka pekee na wale ambao anatarajia kuwa watampa majibu yatakayomwezesha kuyafikia malengo yake. Hivyo, mbinu hii ilisaidia sana katika uteuzi wa sampuli ambayo si ya kubahatisha kwani iliwapa watafiti uhuru wa sampuli ambayo ilikuwa na wahusika waliokuwa na sifa walizozitaka.

Katika ukusanyaji wa data, utafiti huu ulitumia hojaji za kujazwa pamoja na mahojiano ya ana kwa ana kwa kutumia maswali ya dodoso kama mwongozo. Wahadhiri wanne walishiriki katika kujibu maswali yaliyoandaliwa kwa ajili ya kuzibaini changamoto za kipragmatiki miongoni mwa wanafunzi wanaowafundisha. Kwa upande mwingine, wanafunzi 200 wa Kiswahili kutoka mwaka wa pili na wa tatu nao walipewa hojaji kwa kulenga kukusanya changamoto wanazokabiliana nazo katika matumizi yao ya Kiswahili. Uteuzi wao ulizingatia kuwa ndio waliokuwa na uwezo wa kujibu maswali yanayoegemea kipengele cha pragmatiki. Aidha, utafiti huu ulitumia mbinu ya mahojiano ili kuweza kujiridhisha na maoni ya watoataarifa kuhusu maswali yaliyoulizwa. Kwa hivyo, zaidi ya wahadhiri wanne wa Kiswahili, wanafunzi 20 kati ya wanafunzi 200 waliopewa hojaji ndio walioshirikishwa katika mahojiano ya utafiti huu. Uteuzi wa wanafunzi hawa ulizingatia uwezo waliokuwa wameudhihirisha katika somo la mbinu za mazungumzo na maandishi ambalo hufundishwa katika mwaka wa kwanza. Wanafunzi waliopata walau alama 70 kwa 100 ndio walioteuliwa kushiriki katika mahojiano. Watafiti waliamini kwamba uwezo wao wa kimazungumzo na kimaandishi ungewawezesha kujibu kikamilifu maswali amabayo wangeulizwa.

#### **4.0 Matokeo ya Utafiti**

Kutokana na matokeo ya utafiti huu, wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda wanakabiliwa na changamoto mbalimbali katika matumizi yao ya Kiswahili. Kulingana na data zilizokusanywa, wahadhiri na wanafunzi wa Kiswahili walionesha kuwa changamoto nyingi wanazokutana nazo katika matumizi yao ya Kiswahili ziliyegemea katika matumizi ya lugha ya staha kama vile kumwamkia mtu mkubwa kiumri na kumuaga, uombaji huduma, na kumshukuru aliyewatendea mema au kuwahudumia. Kwa kuwa walimu ndio mfano mzuri wa kuigwa na wanafunzi wao, watafiti waliwauliza kwanza ikiwa ni jambo muhimu kwa wanafunzi kuzingatia lugha ya staha katika mawasilino yao. Majibu waliyoyatoa

yalibainisha kuwa staha ni kipengele muhimu cha mawasiliano ya kawaida ya kila siku na kuwa hutumiwa kama kigezo cha kupimia ikiwa mtu alilelewa vizuri au la. Yafuatayo yalielezwa kwa mfano na mwalimu mmoja:

Lugha inayotumiwa na mtu katika mawasiliano ya kawaida, inasaidia kuamua mtu huyu ni nani, anatoka wapi na mienendo yake ni ipi. Lugha hiyo inahakikisha ikiwa mtu huyo anajali kanuni za kijamii ambazo husaidia kuweka bayana au kufafanua ujumbe anaolenga kuutoa. Kwa meneno mengine, wakati wa kuamkiana kwa mfano, mzungumzaji au msikilizaji anaweza kutambua kwa urahisi ikiwa mwenzake anajali matumizi ya lugha ya staha au la. Hivyo, lugha ya staha inafaa kuzingatiwa na wanafunzi wetu katika mawasiliano yao.

Kulingana na maelezo haya, ni dhahiri kuwa walimu walielewa kuwa wanafunzi wao wanapaswa kutumia lugha ya staha katika mawasiliano yao. Kwa kulifafanua jambo hili, walimu walitilia mkazo kuwa mara nyingi lugha ya staha inayotumiwa na mtu ndiyo inayoamua ikiwa mtu huyo ana maadili kwa kiasi fulani. Baada ya walimu kutoa majibu yao kuhusu nafasi ya lugha ya staha katika mawasiliano ya wanafunzi wao, watafiti waliongeza swali jingine lililolenga kujua ikiwa wanafunzi wao wanazingatia ipasavyo matumizi ya lugha ya staha katika mawasiliano yao na walimu. Majibu waliyoyatoa yalidhihirisha kwamba baadhi ya wanafunzi hawajali matumizi ya lugha ya staha na kuwa ni mtindo unaotumiwa na wanafunzi wachache. Mathalani, mwalimu mmoja alitoa jibu lifuatalo:

Si jambo la kushangaza ukimwona mwanafunzi akimwendea mwalimu au kiongozi yeyote kwa ajili ya kumuomba huduma na kumwamkia kwa kutumia lugha ya watu wa rika moja. Ni kwa nadra wanafunzi wetu kutumia maneno ya kuonesha heshima au lugha ya staha kama vile shikamoo, samahani, tafadhali na mengineyo.

Kutokana na jibu la mwalimu huyu, ni dhahiri kwamba baadhi ya wanafunzi wa Kiswahili wanakabiliwa na changamoto ya kuzingatia lugha ya staha wanapowasiliana na watu wakubwa kiumri na/au viongozi wao. Matumizi ya lugha kwa kuzingatia umri, cheo au wadhifa humtaka mtumiaji ateue maneno maalum na kuacha mengine katika mawasiliano yake. Kwa kawaida, hiki ni kigezo muhimu cha kutambua mtu aliye na umahiri katika matumizi ya lugha husika. Hivyo, watoataarifa ambao ni wanafunzi walikumbwa na changamoto ya kujali matumizi ya maneno maalum ambayo ni kielelezo cha matumizi sahihi ya Kiswahili kati ya mdogo na mkubwa au yale yanayoweza kutokea kati ya mtu wa kawaida na kiongozi.

Aidha, matokeo ya utafiti yanaonesha kwamba watoataarifa wanafunzi wanakabiliwa na changamoto ya kuhamisha mitindo mbalimbali kutoka Kinyarwanda kwenda Kiswahili. Miongoni mwa mitindo ya lugha iliyohamishwa kutoka L1 hadi L2 ni ile ya kusalimiana na kumuaga mtu. Majibu yaliyopatikana kutokana na hojaji za wanafunzi wa Kiswahili yalibainisha kwamba kipengele cha

matumizi ya salamu na kuaga kinazingatia uhamishaji wa mitindo ya lugha kutoka Kinyarwanda hadi Kiswahili kama inavyoonekana katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali Na. 4.1: Matumizi ya Lugha ya Salamu na Kuaga**

Maswali kwa wanafunzi	Majibu	Idadi	%
Ukikutana na mtu mkubwa kiumri unafanya nini?	Natanguliza salamu	60	30
	Nampa nafasi ya kutanguliza salamu	140	70
Ukimsalimu mtu huyo unatumia neno gani kati ya haya?	Hujambo	0	0
	Hamjambo	130	65
	Shikamoo	70	35
Ukimuaga mtu huyo unatumia neno lipi kati ya haya?	Kwa heri	0	0
	Kwa herini	200	100
Kwa nini unachagua neno hilo?	Heshima	90	45
	Mtindo unoakubalika katika Kiswahili	0	0
	Ni mtindo wa kawaida katika lugha yangu ya kwanza	110	55

**Chanzo:** Data ya Uwandani, 2023

Kulingana na majibu yaliyotolewa katika Jedwali Na. 4.1, watoataarifa wanafunzi walieleza wazi kwamba kitendo cha kwanza wanachokifanya wakikutana na mtu ni kumsalimu. Baada ya kusalimu wanaongea na kabla ya kuachana wanamuaga. Wanafunzi hawa pia walionesha maneno wanayoyatumia katika vitendo hivyo. Lengo la maswali yaliyoulizwa katika Jedwali Na. 4.1 lilikuwa kubainisha nani anatanguliza salamu, na anatumia maneno gani kumwamkia na kumuaga mtu huyo. Kulingana na majibu yaliyotolewa, watoataarifa wanafunzi wanajua kile ambacho wanatakiwa kufanya wakati wanapokutana na mtu mkubwa kiumri na kile kinachofanyika baada ya mawasiliano yao. Asilimia 30 ya wanafunzi walionesha kwamba wakati wanapokutana na mtu mkubwa kiumri, bila kusita wanatanguliza salamu ilhali wengine, yaani asilimia 70 walionesha kuwa wanamsubiri mtu huyo atangulize salamu. Kwa hivyo, ni wazi kwamba wanafunzi hawa wanakabiliwa na changamoto ya kujua mtu anayetanguliza salamu kati ya mkubwa na mdogo. Kwa kawaida katika utamaduni wa Kiswahili, mdogo ndiye anayeamkia mkubwa, wakati katika utamaduni wa Kinyarwanda mkubwa ndiye anayemsalimu mdogo. Hata hivyo, jambo zuri lililogunduliwa katika utafiti huu ni kuwa watoataarifa wanafunzi

wanajua maneno yanayopaswa kutumiwa wakati wa kusalimu na kuamuga mtu mkubwa kiumri.

Aidha, majibu yaliyotolewa katika Jedwali Na. 4.1 yalibainisha kuwa idadi kubwa ya wanafunzi hufanya makosa ya kipragmatiki katika mawasiliano yao. Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kwamba asilimia 65 ya wanafunzi huchagua kutumia neno *hamjambo* badala ya neno *hujambo* ambalo ndilo sahihi katika kumwamkia mtu mmoja. Asilimia 35 walichagua neno *shikamoo* ambalo kwa kawaida linatumiwa wakati wa kumsalimu mtu mkubwa kiumri au mwenye cheo cha juu. Hivyo, majibu ya wanafunzi yamekuwa kielelezo kizuri cha mazoea yao wanapokutana na mtu mkubwa kiumri.

Halikadhalika, mahojiano yaliyofanywa kwa kuhusisha wanafunzi yalionesha kwamba wao hutumia neno *hamjambo* wakifikiria kuwa ndilo neno sahihi la kuonesha heshima kwa mtu mkubwa kiumri. Kutokana na matumizi ya neno hilo, ni dhahiri kuwa wanafunzi waliathiriwa na matumizi ya idadi ya wingi ambayo ndiyo inayotumiwa katika salamu zao, pale mtu mdogo kiumri akimsalimu yule anayemzidi umri. Kulingana na utamaduni wa Wanyarwanda, maneno kama *mwaramutse* (mmeamkaje), *mwiriwe* (mmeshindaje), na *muraho* (habari za siku nyingi), hutumika pale mtu mdogo kiumri anapomjulika hali mtu mkubwa au mtu mwenye wadhifa wa juu. Maneno hayo yote yanatumia kiambishi cha wingi cha nafsi ya pili *mu-* ambacho ni kielelezo cha heshima kwa mtu mkubwa.

Pia, utafiti huu ulibaini kwamba wanafunzi hawajali matumizi sahihi ya maneno ya kuagana. Matokeo katika Jedwali Na. 4.1 yanabainisha kwamba wanafunzi wote walioulizwa neno sahihi la kutumiwa wakati wa kuaga kati ya *kwa heri* na *kwa herini*, walichagua neno *kwa herini* kumuaga mtu mmoja. Hivyo basi, majibu waliyoyatoa yalitokana na kuathiriwa pia na mitindo ya Kinyarwanda ya kuagana ambapo kiambishi cha wingi cha nafsi ya pili hutumiwa kumuaga mtu mmoja kama ishara ya heshima kwake. Maneno kama *mwirirwe* (siku njema), *muramuke* (alamsiki) *murabeho* (kwa herini na *tuzabonana ejo* (tuonane kesho) ni mifano ya matumizi ya idadi ya wingi katika kumuaga mtu mwenye heshima katika utamaduni wa Wanyarwanda, na maneno hayo yanatumia kiambishi cha wingi *mu* kama tulivyoeleza hapo juu.

Changamoto nyingine ya kuhamisha mitindo ya L1 hadi L2 ilijitokeza katika mitindo ya kuomba huduma inayostahili na kumshukuru mtoa huduma hiyo. Katika jedwali Na. 4.2 tunaonesha lugha inayotumiwa na wanafunzi wakati wa kuomba huduma na ile wanayoitumia baada ya kupewa huduma waliyoiomba. Vilevile, sababu za kutumia mitindo waliyoichagua nazo zimebainishwa:

**Jedwali Na. 4.2: Matumizi ya Vipengele vya Staha katika Mawasiliano ya kila Siku ya Wanafunzi**

Maswali	Majibu	Idadi	%
Ukitaka kuomba huduma unayostahili kupewa katika ofisi ama sehemu nyingine unatumia maneno yapi?	i. Nawaomba msaada wa....	70	35
	ii. Nipe msaada wa...	0	0
	iii. Tafadhali nawaomba msaada wa....	100	50
	iv. Nakuomba msaada wa....	10	5
	v. Tafadhali nakuomba msaada wa....	20	10
2. Kwa nini unachagua maneno haya ?	i. Kwa uzoefu tu	80	40
	ii. Yanatumiwa katika lugha ya Kinyarwanda	110	55
	iii. Ni mtindo unaotumiwa katika Kiswahili	10	5
3. Ukipewa huduma na mtu mmoja katika ofisi fulani ama sehemu nyingine, unatumia neno gani kwa kumshukuru?	i. Asanteni	100	50
	ii. Asante	7	3.5
	iii. Shukrani	80	40
	iv. Nakushukuru	13	6.5

**Chanzo:** Data ya Uwandani, 2023

Kulingana na majibu yaliyotolewa katika Jedwali Na. 4.2, imebainika kuwa wanafunzi hutumia miundo tofuti wanapooomba huduma au wanaposhukuru kwa ajili ya huduma iliyotolewa. Aidha, matokeo yanaonesha kwamba idadi kubwa ya wanafunzi walichagua miundo yenye kiambishi cha wingi wa-. Kikundi cha maneno *nawaomba msaada wa...* kilichaguliwa na asilimia 35 ya wanafunzi wakati asilimia 50 walipendelea *tafadhali nawaomba msaada wa...* Miundo hii ilitumiwa na wanafunzi wengi kuliko miundo mingine, kwani asilimia 5 waliegemea katika matumizi ya *nakuomba msaada wa...* ilhali asilimia 10 walichagua *tafadhali nakuomba msaada wa....*

Uchunguzi wa matumizi ya vikundi vya maneno vilivyopendelewa zaidi na wanafunzi unadhihirisha kuwa walivutiwa na miundo yenye neno *tafadhali* ambalo liliambatishwa na matumizi ya kiambishi cha wingi wa-. Hivyo basi, wanafunzi hawa walionesha kuwa walifahamu umuhimu wa neno *tafadhali* katika kuonesha staha kwa mtu wanayemuomba huduma. Kuambatisha matumizi ya neno *tafadhali* pamoja na matumizi ya kiambishi cha idadi ya wingi wa- ilikuwa njia ya kuthibitisha heshima wanayostahili kumpa mtu anayewatolea huduma. Hali hii ndiyo iliyowafanya wanafunzi (asilimia 50) wachague muundo wa *tafadhali*

*nawaomba msaada wa... ilhali asilimia 10 walichagua muundo wa tafadhali nakuomba msaada wa....*

Vilevile, matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kwamba lugha ya kimaongezi ya wanafunzi hutofautina na mtindo wao katika maandishi. Katika mahojiano yaliyofanywa, watafiti waligundua kuwa baadhi ya wanafunzi hawajali matumizi ya neno *tafadhali* kama alivyoeleza mwalimu mmoja:

Wanafunzi wetu huvutiwa na miundo ya lugha ya staha wanapoikuta katika maandishi. Katika mazungumzo yao, wao hukumbuka kutumia maneno kama *tafadhali*, *samahani*, *kumradhi* kwa mara chache. Wakiulizwa maana au matumizi ya maneno hayo katika kifungu cha maandishi watakujibu kuwa wanayafahamu vizuri lakini usishangae ukiongea nao kwani ni wachache watakaokumbuka kuyatumia maneno hayo kama ishara ya kujali matumizi ya lugha ya staha.

Kutokana na maelezo ya mwalimu huyu, ni dhahiri kwamba wanafunzi wanafahamu umuhimu wa lugha ya staha katika kuomba huduma, msamaha au radhi. Maelezo ya walimu yalibainisha kuwa wanafunzi hutumia moja kwa moja vitenzi vinavyozingatia maana ya kile wanachohitaji kusema kama vile *nisamehe*, *nipe ruhusa*, na *naomba ruhusa*. Walimu walizidi kueleza kuwa wanafunzi wao wanapokutana na maneno ya kuashiria lugha ya staha katika maandishi huvutiwa sana na kuiona kama kielelezo kizuri cha mtu aliye na umahiri katika mawasiliano. Hata hivyo, walimu walithibitisha kwamba wanafunzi wao hawakumbuki mara nyingi kutumia lugha hiyo ya staha wanapongea. Aidha, walimu wote waliweka bayana kuwa umilisi wa lugha ya maandishi na mazungumzo kwa wanafunzi wao hutofautiana. Walieleza kuwa katika maandishi, wanafunzi hupata muda wa kutosha kwa kufikiria kile wanachotakiwa kuandika, ilhali, katika mazungumzo, uzoefu wao mdogo huwafanya wasitumie miundo sahihi hata kama wanaifahamu. Halikadhalika, matokeo ya utafiti huu katika Jedwali Na. 4.2 yalibainisha kuwa wanafunzi walipendelea kutumia neno *asanteni* bila kujali ikiwa wanamshukuru mtu mmoja, watu wawili au zaidi. Vilevile, neno *shukrani* nalo liliweza kutumiwa na wanafunzi bila kuzingatia ikiwa anayeshukuriwa ni mtu mmoja au zaidi. Asilimia 3.5 walioegemea katika matumizi ya neno *asante* pamoja na asilimia 6.5 walioegemea katika matumizi ya neno *nakushukuru* ni kielelezo kamili kinachotudhihirishia kuwa wanafunzi watoataarifa wanafikiria kuwa idadi ya umoja haifai kutumiwa katika mawasiliano kuonesha heshima kwa mtu anayetoa huduma. Idadi kubwa ya wanafunzi walichagua kutumia maneno *asanteni* (50%) na *shukrani* (40%) kama njia za kuonesha heshima kwa mtu anayewahudumia. Kulingana na matumizi ya neno *shukrani*, matokeo ya utafiti yalionesha kwamba wanafunzi waliathiriwa na hali yao ya kujumuisha kanuni ya wingi katika lugha ya Kiswahili. Silabi *-ni* inayojitokeza mwishoni mwa neno *shukrani* ilichukuliwa kama kiambishi *-ni* cha wingi kiasi kwamba waliliweka katika fungu moja na neno *asanteni*.

### 5.0 Ufafanuzi wa Matokeo

Uchunguzi wa matokeo ya utafiti huu ulibaini kuwa wanafunzi walikuwa na taratibu mbili tofauti wanazozitumia kwa ajili ya kufanikisha mawasiliano yao. Utaratibu wa kwanza ni ule wa kumuamkia mtu mkubwa kiumri au mtu mwenye wadhifa wa juu kwa kutumia kiambishi cha wingi cha nafsi ya pili. Utaratibu wa pili ni ule wa kuzingatia maneno mwafaka ya kuonesha staha kama yanavyoagizwa na utamaduni wa Waswahili. Utaratibu wa kwanza unatumiwa na wanafunzi wengi ilhali utaratibu wa pili unatumiwa na wanafunzi wachache. Utafiti huu umedhihirisha kuwa wanafunzi wengi hawaheshimu desturi za Waswahili kwa kuwa wao ndio wanaoanzisha maamkizi wanapokutana na mtu mkubwa kiumri. Hivyo, ni wazi kwamba wanafunzi wenyewe hukabiliwa na changamoto ya kuzingatia mazoea na utamaduni wa Kinyarwanda katika mawasiliano yao. Kutoweza kufanikiwa katika matumizi ya maneno sahihi wanayoyafahamu katika shughuli zao za kuomba huduma, msamaha au radhi ni ishara kwamba wanafunzi hawa hukumbwa na changamoto kubwa ya kukosa mazingira mwafaka yanayoweza kuwasaidia kuimudu lugha ya Kiswahili na kuitumia ipasavyo kulingana na miktadha tofauti.

Matumizi ya maamkizi ya Kiswahili hutofautiana na yale ya Kinyarwanda. Tofauti ya kwanza inalenga mtu wa kutangulia kutoa salamu kati ya mdogo na mkubwa kiumri. Kwa kawaida, katika utamaduni wa Kiswahili, mdogo ndiye anayetanguliza salamu kwa mtu mkubwa, wakati katika utamaduni wa Kinyarwanda mkubwa ndiye anayemsalimu mdogo. Tofauti ya pili ni vigezo vya staha vinavyotumiwa katika matumizi ya maamkizi. Katika utamaduni wa Kiswahili kuna salamu za kipekee zinazotumiwa na wadogo kwa wakubwa kinyume na utamaduni wa Kinyarwanda unaohimiza matumizi ya viambishi vya wingi kwa kurejelea mtu mmoja anayestahili kupewa heshima. Hali hii ndiyo iliwafanya wanafunzi wengi waegeme kuwa mwenendo sahihi ni wa mtu mdogo kumsubiri mtu mkubwa kutanguliza salamu kwake. Asilimia 70 walisema kuwa wakikutana na mtu mkubwa kiumri wananyamaza, kimya hicho kinakuwa ishara ya kumwachia mtu mkubwa nafasi ya kuwasalimu kama njia ya kuonesha heshima kwake. Idadi kubwa ya wataoataarifa walionesha kuwa wanafunzi wengi huangukia katika mtego wa kuchanganya taratibu za Wanyarwanda na zile za Waswahili. Wao hawajui kuwa wadogo ndio wanaopaswa kutanguliza salamu wakati wanapokutana na wakubwa kiumri kama ilivyo katika utamaduni wa Waswahili.

Utumiaji wa viambishi vya wingi wakati wa kumrejelea mtu mmoja ni mojawapo ya makosa ya uhamishaji wa mtindo kutoka L1 hadi L2. Kwa kawaida, viwakilishi nafsi huru vya nafsi ya pili na viambata huwa na matumizi ya kipragmatiki ya kipekee katika Kinyarwanda kwani huonesha heshima kwa mtu mkubwa. Mtindo huu ndio ulioathiri matumizi ya jumla ya viambishi vya wingi vya nafsi ya pili wakatika mawasiliano ya wanafunzi. Matalani, wanafunzi walipendelea kutumia *nawaomba msaada wa.... badala ya nakuomba msaada wa....* Idadi ndogo ya

watoataarifa wanafunzi walioonesha kwamba matumizi ya maneno *nakushukuru* na *asante* ndiyo yanayostahili kutumika katika kitendo cha kumshukuru mtu mmoja. Hivyo, wanafunzi wengi huathiriwa na L1 katika uombaji na kushukuru kwa huduma iliyotolewa. Kutokana na hali hii tunaweza kusema pia kuwa mawasiliano ya wanafunzi hawa katika kipengele cha staha yanaathiriwa sana na vigezo vya kisoshoutamaduni vya mazingira ambamo wanaishi.

Aidha, matumizi ya viambishi kwa njia isiyo sahihi pale wanafunzi wanapoongea na wahadhiri wao ama watu wengine wenye heshima katika ofisi mbalimbali yalitamalaki kwa kuwa huo ndio mtindo waliouzoea katika lugha yao ya kwanza. Badala ya kutumia hali ya umoja katika kusalimu, kuaga na kushukuru, idadi kubwa ya wanafunzi wanatumia hali ya wingi, yaani maneno kama *hamjambo*, *kwa herini* na *asanteni* wakirejelea mtu mmoja. Kwa kawaida, utaratibu huu unakinzana na utamaduni wa Waswahili kwa sababu Kiswahili kinahimiza matumizi ya viambishi kulingana na idadi ya watu wanaorejelewa, tofauti na hali ilivyo katika Kinyarwanda. Ikiwa ni mtu mmoja, viambishi vya umoja vinatumiwa na ikiwa ni wingi viambishi vya wingi ndivyo hutumiwa katika Kiswahili. Kwa upande mwingine, sarufi ya Kinyarwanda inawaelekeza watumiaji wazingatie kiambishi cha umoja kumrejelea mtu mmoja na kiambishi cha wingi kuwarejelea watu wengi; lakini, kimuktadha, viambishi vya wingi vya nafsi ya pili hutumiwa kwa kuheshimu mtu mkubwa kiumri ama mtu mwenye wadhifa wa juu.

Aidha, maelezo ya hapo juu yanathibitisha kuwa wanafunzi Wanyarwanda huathiriwa zaidi na vipengele kadhaa vya mchakato mwachano kwa kujihusisha na utamaduni pamoja na mazoea ya matumizi ya mitindo ya lugha yao ya kwanza. Katika Kiswahili, hakuna tofauti kati ya matumizi ya viambishi vya kisarufi na maana zinazoashiriwa na viambishi hivyo. Ikitokea kwamba mzungumzaji anatakiwa kutumia lugha ya staha kuna maneno maalum yanayozingatiwa katika Kiswahili, ilhali Kinyarwanda kinahimiza matumizi ya kanuni za kijamii kwa kuhusisha matumizi ya kiambishi cha nafsi ya pili cha wingi kumrejelea mtu mmoja kama lugha ya staha. Hivyo basi, kosa linalofanywa na wanafunzi wengi Wanyarwanda wanapotumia viambishi vya wingi kumrejelea mtu mmoja, hutokana na uhamishaji wa taratibu na kanuni za utamaduni wa Kinyarwanda katika mawasiliano yao ya Kiswahili. Kosa hili linahusiana moja kwa moja na Nadharia ya Urekebishaji Mawasiliano, pale ambapo mzungumzaji wa lugha ya pili anajenga umbali ama ukaribu na msikilizaji.

Kulingana na Nadharia ya Urekebishaji Mawasiliano, vipengele vinavyoathiri mawasiliano ni utamaduni, itikadi na imani. Katika utafiti huu baadhi ya wanafunzi walijinasibisha na utamaduni wa Waswahili walipochagua kutumia maneno maalum kama lugha ya staha ingawa idadi kubwa walichukua mwelekeo tofauti na ule wa wazawa wa lugha ya Kiswahili kwa kushindwa kuchagua mtindo sahihi unaofaa katika mawasiliano yao. Vipengele vya kisoshoutamaduni vya mzungumzaji ndivyo vilivyowaathiri wanafunzi Wanyarwanda kwani mazingira



wanamoishi hayawaruhusu kutumia ipasavyo Kiswahili kama lugha ya mawasiliano yao ya kila siku. Fursa zilizopo za kutumia Kiswahili ni chache kwani wanapotoka shuleni hutangamana zaidi na watu wasiojua Kiswahili. Hivyo, wao hutumia mikakati makutano kwa nadra kutokana na uzoefu wao mdogo wa kutumia Kiswahili. Mikakati mwachano ya kimazungumzo ndiyo wanayoitumia zaidi kuonesha kuwa wanaielewa mienendo na mitazamo ya kijamii ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Giles (1973) anaeleza kwamba mikakati hiyo ya mwachano na makutano ndiyo inayochangia sana katika kuhamisha ama kutohamisha mitindo fulani kutoka lugha moja hadi nyingine.

### 6.0 Chanzo cha Changamoto za Kipragmatiki

Si rahisi kugundua kila mara asili ya kosa linalofanywa. Kama ilivyodhihirishwa katika makala haya, wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda wanakutana na vikwazo mbalimbali vya kipragmatiki. Kwa lengo la kutambua ikiwa walimu na wanafunzi wa Kiswahili wanajua vyanzo vya changamoto ambazo hujitokeza katika mawasiliano yao ya kila siku, tuliwauliza maswali. Kupitia Jedwali Na. 6.1, wanafunzi na walimu walidhihirisha asili ya vikwazo vya kipragmatiki ambavyo wanakutana navyo katika mawasiliano :

**Jedwali Na. 6.1: Vyanzo vya Vikwazo vya Kipragmatiki kwa Wanafunzi**

Vyanzo vya vikwazo vya kipragmatiki vilivyodhihirishwa	Wanafunzi				Walimu			
	Ndiyo	%	Hapana	%	Ndiyo	%	Hapana	%
Kujifunzia Kiswahili nje ya utamaduni wake	195	97.5	5	2.5	4	100	0	0
Kuanza kujifunza Kiswahili katika ngazi za juu	186	93	14	7	3	75	1	25
Ukosaji wa kielelezo cha kufuatilia	171	85.5	29	14.5	1	25	3	75
Vyanzo vingine	173	86.5	27	13.5	4	100	0	0

**Chanzo:** Data ya Uwandani, 2023

Kwa kurejelea Jedwali Na. 6.1, wanafunzi wa Kiswahili walidhihirisha vyanzo vya vikwazo vya kipragmatiki ambavyo wanakutana navyo katika mawasiliano yao ya kila siku: kujifunzia Kiswahili nje ya utamaduni wake, kuanza kujifunza Kiswahili katika ngazi za juu, na ukosaji wa kielelezo cha kufuatilia. Mbali na vyanzo vilivyoorodheshwa katika Jedwali Na. 6.1, watoataarifa waliongeza vyanzo vingine kama fursa chache za kutumia Kiswahili, mazingira ya ujifunzaji Kiswahili pamoja na uzoefu mdogo wa kuzungumza lugha hii.

Miongoni mwa vyanzo vilivyobainishwa na walimu pamoja na wanafunzi, utamaduni ulichukua nafasi kubwa. Watoataarifa walioegemea katika hoja hii

walionesha kwamba vipengele vya utamaduni wa Kinyarwanda vinavyohusiana na vile vya Kiswahili havileti changamoto kubwa katika matumizi ya Kiswahili. Walitoa mfano, kama pale ambapo kila mtumiaji wa lugha ya Kiswahili hukumbuka kumshukuru anayemtotea huduma. Vilevile, kukumbuka kujuliana hali baina ya watu wanaokutana ni jambo la kawaida katika mawasiliano ya watumiaji wa Kiswahili na Kinyarwanda. Watoataarifa wanafunzi walieleza pia umuhimu wa kuamkiana na kuagana baina ya watu. Hata hivyo, kuna vipengele vingine vya kiutamaduni ambavyo huwatatiza wanafunzi wanapotumia Kiswahili. Hali hii hutokea zaidi pale ambapo mienendo na mitazamo ya Waswahili hutofautiana na ya Wanyarwanda. Matokeo ya utafiti huu yalionesha kwamba wanafunzi wengi walishindwa kufuata taratibu za Waswahili katika matumizi sahihi ya miundo ya lugha ya kusalimiana, kuagana, kuomba radhi na kushukuru. Kwa hivyo, vyanzo vilivyobainishwa hapo juu vilionekana kuwa na uhusiano wa moja kwa moja na mazingira ya ujifunzaji wa Kiswahili na utamaduni wa mahali ambapo mawasiliano ya wanafunzi hutokea.

Aidha, watoataarifa walieleza kwamba kuanza kujifunzia Kiswahili katika ngazi za juu nako kunachangia katotumia Kiswahili fasaha kulingana na mazingira au miktadha ya utamaduni wa Waswahili. Nchini Rwanda wanafunzi hukutana na Kiswahili kwa mara ya kwanza wanapofikia shule za sekondari. Wakati huu wanafunzi hawa huwa wameishazoea mitindo ya mawasiliano ya lugha walizojifunza kuanzia shule za chekechea. Kwa mfano, Kinyarwanda na Kifaransa hutilia mkazo matumizi ya idadi ya wingi kama lugha ya heshima ikiwa mzungumzaji anawasiliana na mtu mkubwa kiumri ama mwenye wadhifa wa juu. Hivyo, lugha hizi huwaathiri wanafunzi Wanyarwanda wanapotumia Kiswahili katika mawasiliano yao. Katika makala haya, watafiti walijikita katika uchunguzi wa athari za matumizi ya Kinyarwanda katika Kiswahili kama lugha zenye mnasaba mmoja, kama ilivyoelezwa hapo juu.

Wanafunzi wa Kinyarwanda wanapoanza kujifunza Kiswahili hukosa mazingira mwafaka ya kuwarahisishia na kuendeleza ujifunzaji wao kwani wanapofika nyumbani huwa hawana mtu mwingine wa kuwasiliana naye kwa Kiswahili. Hivyo basi, ukosefu wa fursa za kutumia Kiswahili pamoja na watu wenye umahiri wa kutumia lugha hiyo katika mazingira mbalimbali ni chanzo kingine cha changamoto za kipragmatiki kwa wanafunzi. Kutokana na matokeo ya utafiti huu, tunathibitisha kuwa umilisi wa kipragmatiki huendelezwa zaidi ikiwa mtumiaji wa lugha huzipata fursa mbalimbali za kuitumia lugha husika katika mazingira na miktadha tofauti ya maisha yake. Jamii ndiye mwalimu mzuri wa kuendeleza umilisi huu wa kipragmatiki kuliko anavyoweza kufanya mwalimu wa darasani.

Halikadhalika, vielelezo vizuri vya kuigwa ni wazawa wa lugha husika kwa sababu wao wana umilisi wa lugha yao na wanafahamu vizuri mitindo mbalimbali ya matumizi ya lugha yao kulingana na hali na mazingira ya mawasiliano. Vielelezo hivi vya kuigwa hutoa pia mchango mkubwa katika maendeleo ya kipragmatiki kwa

wanafunzi wa lugha ya pili. Kutumia mazungumzo kwa kuzingatia vielelezo vilivyopo huweza kuwa suluhisho la kuepuka makosa ya hapa na pale, yakiwamo matumizi yasiyo sahihi ya lugha husika. Hivyo, makosa mbalimbali yaliyofanywa na wanafunzi wa Kiswahili yalitokana na ukosaji pia wa kielelezo ambapo waliweza kuhamisha taratibu za Kinyarwanda hadi katika Kiswahili kama ilivyokwishaeleza.

### 7.0 Hitimisho

Makala haya yamechunguza changamoto za kipragamatiki zinazowakumba wanafunzi wa Kiswahili nchini Rwanda. Imebainika kuwa changamoto nyingi wanazokutana nazo hujitokeza pale wanapoathiriwa na mitindo ya lugha ya Kinyarwanda katika mawasiliano yao ya kutumia Kiswahili. Ingawa walimu wao wanawahimiza kutumia Kiswahili fasaha, kuna makosa wanayoyafanya kutokana na ukosefu wa miktadha mbalimbali ya kimatumizi ya Kiswahili. Aidha, athari za lugha yao ya kwanza huendelea kuwa kikwazo kikubwa kinachowafanya wanafunzi hawa wasitumie Kiswahili fasaha katika mawasiliano yao. Utafiti huu umebaini kwamba wanafunzi wa Kiswahili huathiriwa na mitindo mbalimbali ya Kinyarwanda inayohamishwa moja kwa moja hadi Kiswahili.

Kwa kuzingatia matokeo ya utafiti huu, ni lazima wanafunzi wa Kiswahili wafahamu kuwa ingawa lugha ya Kiswahili ina uhusiano wa karibu na lugha ya Kinyarwanda, lugha hizi zina vipengele vya kiisimu vinavyotofautiana kimatumizi, hususan katika kigezo cha kipragmatiki. Kuwa makini katika matumizi ya vipengele vya kiisimu pamoja na maneno yanayoshiria mienendo mizuri ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili au staha ni jambo la kutiliwa mkazo katika mawasiliano ya wanafunzi. Jambo hili likizingatiwa litawasaidia kuepuka makosa ya kimatumizi yanayotokana na athari za lugha ya kwanza katika mawasiliano yao. Njia nyingine inayoweza kuwasaidia wanafunzi hawa ni kufuata vielelezo wanavyoweza kusikia kutoka kwa watumiaji wa Kiswahili walio na umahiri wa kimatumizi au kufuatilia idhaa mbalimbali za redio, runinga au nyenzo nyingine za kidijiti. Walimu wao nao wanatakiwa kutilia mkazo kukuza na kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali ya maisha ya wanafunzi kwani utafiti huu umebaini kuwa darasani ndiyo fursa muhimu ya wanafunzi hawa ya kutumia Kiswahili.

### Marejeleo

- Allami H. na Naeimi, A. (2011) "A Cross-Linguistic Study of Refusals: An Analysis of Pragmatic Competence Development in Iranian EFL Learners." *Journal of Pragmatics*, Juz. 43 (1): 385-406. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1016/j.pragma.2010.07.010>. Ilisomwa tarehe 4/5/2022
- Bardovi-Harlig, K. & Mahan Taylor, R. (2003) "Introduction to teaching pragmatics". *English Teaching Forum*, Juz. 41(3): 37-39. Inapatikana

- katika [https://americanenglish.state.gov/files/ae/resource\\_files/03-41-3-h.pdf](https://americanenglish.state.gov/files/ae/resource_files/03-41-3-h.pdf). Ilisomwa tarehe 7/12/2022
- Barron, A. (2003). *Acquisition in Interlanguage Pragmatics. Learning How to Do Things with Words in Study Abroad Context*. Amsterdam/Philadelphia: Benjamins.
- Best, W. J. na Kahn, J. V. (2010). *Research in Education*. New Jersey: Person Prentice.
- Blum-Kulka, S. (1997). "DinnerTalk: Cultural Patterns of Socialization in Family". *JNABE*, Juz. 21(4): 100- 117. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1080/15235882.1997.10162716>. Ilisomwa tarehe 30/06/2022
- Brown, P. na Levinson, S. (1992) *Politeness: Some Universal in Language Usage*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Campbell, R. na Wales, R. (1970) "The Study of Language Acquisition". Katika J. Lyons (Mh.) *New Horizons In Linguistics*. Harmondsworth: Penguin.
- Canale, M. (1983) "From Communicative Competence to Communicative Language Pedagogy". Katika J. C. Richards na R. W. Schmidt (Wah.) *Language and Communication*. London: Longman.
- Castillo, E. R. E, (2009) "The Role of Pragmatics in Second Language Teaching". *MA TESOL Collection*. 479. Inapatikana katika [https://digitalcollections.sit.edu/ipp\\_collection/479](https://digitalcollections.sit.edu/ipp_collection/479). Ilisomwa tarehe 02/10/2022
- Cohen, A. (2014) "Towards Increased Classroom Assessment of Pragmatics Ability". *International Journal of Language Testing*, Juz. 4(1):5-25. Inapatikana katika [https://www.ijlt.ir/article\\_114390\\_7d55cc8e8dcd8e2428d567bc5c80147b.pdf](https://www.ijlt.ir/article_114390_7d55cc8e8dcd8e2428d567bc5c80147b.pdf). Ilisomwa tarehe 05/11/2022
- Creswell, J. W. na Clark, P. L. V. (2011). *Designing and Conducting Mixed Method Research*. California: Prentice Hall, Inc
- Crystal, D. (1987). *The Cambridge Encyclopedia of Languages*. New York: Oxford University Press.
- Dewey, J. (1998) "Pragmatism, education, democracy". *The Museum Journal*, Juz. 41(1): 36-50.
- Erton, I. (2007) "Applied Pragmatics and Competence Relations in Language Learning and Teaching". *Journal of Language and Linguistic Studies*. Juz. 3 (1):59-71. Inapatikana katika <https://www.jlls.org/index.php/jlls/article/view/38/38>. Ilisomwa tarehe 15/08/2022
- Giles, H. (1973). "Towards Theory of Interpersonal Accommodation through Language: Some Canadian Data". *Language and Society*, 2(2): 177-192. Inapatikana katika <https://www.jstor.org/stable/4166723>. Ilisomwa tarehe 21/04/2022

- Giles, H. na Bryne, J. L. (1982) "An Integroup Approach to Second Language Acquisition". *Journal of Multilingual and Multicultural Development*, Juz. 3(1):17-40. Inapatikana katika <https://doi.org/10.1080/01434632.1982.9994069>. Ilisomwa tarehe 08/01/2023
- Jung, J. (2017) "Issues in Acquisitional Pragmatics". *Studies in Applied Linguistics & TESOL (SALT)*, Juz. 2(3): 30-64. Inapatikana katika <https://doi.org/10.7916/salt.v2i3.1642>. Ilisomwa tarehe 23/02/2023
- Kasper, G. (1993) "Development Issues in Interlanguage Pragmatics". *SSLA* Juz.18:149-169. Inapatikana katika <https://citeseerx.ist.psu.edu/document?repid=rep1&type=pdf&doi=9eccd7fc5125983ab3f00755a7c8b9fc5d871c42>. Ilisomwa tarehe 06/04/2022
- Leech, G. (1981). *Semantics: The Study of Meaning*. London: Penguin Books, Ltd.
- Massamba, D. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya lugha*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mnata, R. (2014) *Semantiki na Pragmatiki ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Karljamer Print Technology.
- Mugenda, A. G. (2008) *Social Science Research: Theory and Principle*. Nairobi: Applied Research & Training Services.
- Mwangi Ngugi, B. (2007) *Umilisi wa Stadi za Maamkizi katika Ujifunzaji wa Kiswahili*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Nairobi: Kenyatta University.
- Ntawiyanga, S. (2015) *Changamoto za Kimofosintaksia Miongoni mwa Wanafunzi wa Kiswahili wa Shule za Upili Wilayani Muhanga, Nchini Rwanda*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Nairobi: Kenyatta University.
- O'Keefe. (2011) *Introducing Pragmatics in Use*. London: Routledge.
- Omar, A. (1993) "Closing the Conversation in Kiswahili: A Description of the Performance of Native and Non-native Speakers". Selected papers presented at the Annual Meeting of the International Conference on Pragmatics and Language Learning, 2-4 Aprili, Urbana.
- Reigle, L. J. (2011) *The Role of Pragmatics Competence in Second Language Acquisition*. Utah: Utah University.
- Reyes, E. A. (2018) "A Quantitative Meta-Analysis of Neuroimaging Studies of Pragmatic Language Comprehension: In Search of Universal Neural Substrate". *Neuroscience*, 395: 60-88. Inapatikana katika DOI:[10.1016/j.neuroscience.2018.10.043](https://doi.org/10.1016/j.neuroscience.2018.10.043). Ilisomwa tarehe 04/03/2023
- Taguchi, N. (2017) "Interlanguage pragmatics". Katika A. Barron, P. Grundy, na G. Yueguo (Wah.), *The Routledge Handbook of Pragmatics*. Oxford/New York: Routledge. Kur 153-167.
- Taguchi, N. (2011) "Teaching Pragmatics Trends and Issues". *Annual Review of Applied Linguistics*, Juz. 31:289-310. Inapatikana katika DOI: <https://doi.org/10.1017/S0267190511000018>. Ilisomwa tarehe 17/08/2022 .